# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI YA MBOLIBOLI,
S.L.P 108,
**IRINGA.**

**08.03.2023**

**TANGAZO LA KUPATA KIKUNDI/FUNDI (LOCAL FUNDI) KWA AJILI YA UJENZI WA SHULE MPYA YA SEKONDARI YA MBOLIBOLI**
**KAZI Na. LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot Na.1-6**

Shule mpya ya Sekondari ya MBOLIBOLI kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Iringa inawatangazia Vikundi/Mafundi wa fani mbalimbali, wenye nia na uwezo wa kutekeleza kazi zilizooneshwa kwenye jedwali hapo chini kwa ubora na viwango vinavyokubalika.

**MASHARTI KWA MWOMBAJI:**

1. Awe na uzoefu wa kazi za ujenzi zinazofanana na kazi zilizooneshwa.

2. Tangazo hili linatolewa kwa muda wa siku saba (07) tangu tarehe 08/03/2023 hadi tarehe 14/03/2023 na kuwa muda wa utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu utakuwa miezi mitatu (3) tangu siku ya kusaini mkataba.

3. Vikundi/Mafundi watakaoomba kazi hii watapewa kipaumbele zaidi. Pia, waoneshe uzoefu katika kazi za ujenzi wa majengo ya serikali na wawe na orodha ya mafundi wasaidizi wasiopungua kumi (10) kukamilisha kazi kwa wakati.

Scanned with CamScanner

4. Namba ya kazi na orodha ya majengo yatakayojengwa ni kama ifuatavyo:-

| Na. | JENGO | NAMBA YA KAZI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | UJENZI WA JENGO LA UTAWALA | LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot 1 | Miezi 3 |
| 2 | UJENZI WA JENGO LA MAKTABA | LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot 2 | Miezi 3 |
| 3 | UJENZI WA JENGO LA ICT | LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot 3 | Miezi 3 |
| 4 | UJENZI WA MAABARA TATU (03) ZA SAYANSI | LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot 4 | Miezi 3 |
| 5 | UJENZI WA MADARASA NANE (08) | LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot 5 | Miezi 3 |
| 6 | UJENZI WA VYOO ISHIRINI (20) | LGA/IDC/MBOL/2022-2023/NCS/01 Lot 6 | Miezi 3 |

5. Gharama ya Uchukuaji kitabu cha kazi ni **TShs. 20,000/=** kwa kila ombi fedha hii haitarejeshwa. Aidha, Fundi ataruhusiwa kuomba kazi zaidi ya moja lakini atapewa kazi moja tu ambayo atashinda.

6. Kazi za kufanya;
   - Kazi ya msingi (Sub Structure)
   - Kazi ya kujenga kuta (Super Structure)
   - Kazi ya upauaji na kupiga fascia boards
   - Kazi ya kupiga dari(blundering na gypsum boards)
   - Kazi ya umaliziaji -kupiga ripu (Finishing)
   - Kazi ya kuweka sakafu
   - Kazi ya kufunga Milango na madirisha
   - Kazi ya kufunga Madirisha
   - Kazi ya kupiga rangi na mapambo (Painting, decoration and Tyrolean rendering)

7. Vifaa vyote vya ujenzi (Building Materials) vitatolewa na Mwajiri. Fundi atalipwa gharama ya kazi tu (Labour Charge), kwa siku/wiki/mwezi kulingana na makubaliano.

8. Mwombaji awasilishe uthibitisho wa kutokuwa ametenda kosa la kijinai, kuwa na mgogoro na serikali.

9. Fundi aoneshe ujuzi wa kutosha kufanya kazi hizo zilizotajwa na ambatishe nyaraka za kazi alizokwisha fanya (ikiwemo mawasiliano ya alikowahi fanya kazi au mkataba pia awe na kitambulisho cha NIDA au mpiga kura au barua kutoka kwa mtendaji wa mtaa.

10. Mwombaji aambatishe barua ya uthibitisho wa ukazi kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji au Kata anayoishi.

11. Mwaombaji aambatishe picha mbili za Pasport size katika kabrasha la kazi aliyoomba.

Scanned with CamScanner

11. Mwaombaji aambatishe picha mbili za Pasport size katika kabrasha la kazi aliyoomba.

12. Mwombaji atatakiwa kuonesha uthibitisho wa kuwa na vitendea kazi muhimu vitakavyo mwezesha kukamilisha kazi husika (Mfano:- pima maji, mwiko, birigi (Plumb bob), water level, nyundo ndogo za mawe, chepe (Spade), kamba manila za kunyoshea na kusetia na vinginevyo.

13. Kabrasha linaloonesha majengo pamoja na fomu mbalimbali ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Mboliboli zinapatikana katika OFISI YA MKUU WA SHULE YA SEKONDARI YA PAWAGA, kuanzia tarehe 08.03.2023 hadi tarehe 14.03.2023. Muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

14. Maombi ya kazi ya ufundi yaandikwe kwa herufi kubwa yakionesha aina ya kazi uliyoomba, Jina la fundi au Kikundi na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala alama yoyote na yafungwe kwa lakili. Aidha bahasha ifungwe vizuri. Pia, juu ya bahasha iandikwe jina la kazi uliyoomba. Namba ya kazi husika na anuani ya (MKUU WA SHULE, SHULE YA SEKONDARI YA MBOLIBOLI, S.L.P 108, IRINGA). Kisha bahasha iliyofungwa iwasilishwe kwa Mkuu wa shule ya Sekondari Pawaga.

15. Maombi yote katika nakala **halisi moja** na **nakala (copy) moja (1)** yaletwe kwenye Ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Pawaga, S.L.P 108, IRINGA). Muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

16. Siku ya **mwisho** ya kuwasilisha maombi hayo ni tarehe 14.03.2023, saa 5.00 asubuhi na maombi hayo yatafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.

17. Maombi yote ya kazi za ufundi yatakayowasilishwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha hayatapokelewa.

18. Siku ya kutembelea eneo la mradi ili kuwezesha kujaza makabrasha itakuwa tarehe 10.03.2023 (Ijumaa). Mwombaji atatakiwa kufika na kupata maelekezo katika Ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Pawaga kuanzia saa 5.00 kamili asubuhi. Gharama za kutembelea eneo la mradi kila mwombaji atajitegemea.

19. Mwajiri anaweza kufuta maombi yote ya zabuni bila taarifa, ikiwa kutakuwa na sababu ya kufanya hivyo kwa maslahi mapana ya shule.

20. Ufunguzi wa kazi zilizotangazwa utafanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Pawaga. Waombaji wote wanaombwa kuhudhuria katika ufunguzi wa kazi hizo bila kukosa. Aidha, mwajiri halazimiki kumpatia kazi mwombaji wa bei ya chini.

.............................

**Jairos E. Mwakavindi**

**MKUU WA SHULE YA SEKONDARI YA PAWAGA**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI PAWAGA
S.L.P. 1184 IGODIKAFU
IRINGA, TANZANIA

Scanned with CamScanner